# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA AROBAINI NA TATU

**10 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA AROBAINI NA TATU - TAREHE 10 JUNI, 2025

## I. DUA:

## II. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

**547 MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyatambua maeneo yote yanayoathiriwa na maafa na kuweka mkakati wa ziada.

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**548 MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Barabara za Vijijini zilizopo Milimani - Same kwa mawe au zege ili kupunguza gharama za kufanya matengenezo.

**549 MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga uzio katika Shule zilizopo maeneo hatarishi kwa kuwa Shule nyingi za Mkoa wa Lindi hazina uzio.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**550 MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mpango gani kudhibiti uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**551 MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, zipi athari za kisayansi zinazosababishwa na ufugaji wa Samaki kwa njia ya Vizimba.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**552 MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha eneo mahsusi la Viwanda vya kuongeza thamani ya Mazao ya Misitu.

**WIZARA YA MAJI:**

**553 MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini mradi wa maji wa Miji 28 utaanza kutekelezwa Wilayani Mpanda kwa kutoa maji Bwawa la Milala.

**WIZARA YA KILIMO:**

**554 MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji utaanza na kukamilika katika maeneo yote ya Wilaya ya Kalambo yaliyobainishwa kuwa na fursa za kilimo.

**WIZARA YA AFYA:**

**555 MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kwa nini tangu mwaka 2018 hadi leo MSD haijapeleka Majokofu manne ya Mochwari katika Kituo cha Afya Mugeta – Bunda.

**WIZARA YA UJENZI:**

**556 MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, kwa nini Serikali isijenge mitaro katika Barabara ya Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Namtumbo ili kuinusuru isiendelee kuharibiwa na mvua.

**557 MHESHIMIWA STEPHEN LUJWAHUKA BYABATO (BUKOBA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuwatambua Wakandarasi wazawa wanaofanya kazi nzuri ili kuwapa motisha.

**558 MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATTEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami Barabara ya Sepuka - Ndago hadi Kizaga.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**559 MHESHIMIWA YAHYA ALLY MHATA (NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Nanyumbu pamoja na nyumba za Watumishi.

**560 MHESHIMIWA MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB (DIMANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itapeleka magari katika Vituo vya Polisi Wilaya ya Magharibi "B".

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**10 JUNI, 2025** **KATIBU WA BUNGE**